

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, LAIKIPIA WEST
CONSTITUENCY, HELD AT NYAHURURU CATHOLIC HALL**

ON

14TH OCTOBER 2002

By Lillian Bango
Final copy

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, LAIKIPIA WEST CONSTITUENCY, HELD AT
NYAHURURU CATHOLIC HALL ON
14TH OCTOBER 2002**

Present:

1. Com. Isaack Lenaola.

Secretariat Staff in Attendance

1. Francis Wachira - District Coordinator.
2. Achieng Olende - Assistant Programme Officer.
3. Emmah Kamunga - Verbatim Recorder.

The meeting started at 10.00 a.m.

Prayer: Pesacline Kambaria: Lets pray our Father(?) you have given unto us we would to welcome you in our meeting today and you are going to minister unto us gather(Inaudible) then you give glory for the(?) all the people who have gathered this morning. Thank you king of glory we welcome you to begin together with as we.....(?). Thank you the living God because you are going to(?), I pray those in Jesus name(?). Amen.

A lot of noise from the hall.

Francis Wachira: Asante sasa wananchi tutanza mkutano wetu wa leo, kwa sababu Commissioner amekuja kutoka Nairobi na ningetaka kwanza, kabla hatujaanza, nimjulisha wale committee member wamekuwa wanasaidia Laikipia West kutoka wakati tulianza hii mambo ya Katiba mpaka mahali tumefika, sasa ningetaka Miss. Mary Lokiane asimame. Huyu Madam ndio ametusadia sana upande wa sosiam na Rumruti kuokota maoni ya wananchi. Asante Mary. Na ningetaka huyu aseme jina lake.

Mimi naitwa Peter Waweru, mimi ni mmoja wa kamati ya Laikipia West, constituency ya Laikipia West tunaoshugulikia mambo ya Katiba na pia wakati mwingine mimi ni Mwenyekiti wa kamati ile. Asanteni.

Halafu ningetaka kuwaonesha mdogo wangu, Catherine Kathambi, tafadhali simama wakuone, huyu anakaa Nanyuki she is the deputy coordinator Laikipia district. Halafu ningetaka kumjulisha kuna watu delegates wale watatu walichaguliwa hapa Laikipia. Wataenda National Constitutional Conference, na watarepresent maoni ya watu wa Laikipia na tuko na mama mmoja hapa natangetaka asimame tafadhali. Mrs. Tektarina Rebaria, huyu ndio mama anasimamia Laikipia na ndio ataenda kujadilia kwa mwenzi mmoja kutoka tarehe ishirini na nane.

Sasa upandwa Nairobi, kuna the Programme Officer, Mr. Gitonga, ndio ameandamana na Commissioner. Ningetaka kuwaonesha yule anarecord all these proceedings, mama yule pale Emmah, Emmah ndie anarecord kwa microphone. Halafu ningetaka(Inaudible) enyewe yule atatuendelesha hii mambo ya Katiba tafadhali ajitambue.

Com. Isaac Lenaola: Hamjambo.

Audience: Hatujambo.

Com. Isaac Lenaola: Mimi naitwa Isaac Lenaola, mimi ndio Commissioner.

Speaker: Pardon.

Com. Isaac Lenaola: Isaac Lenaola mimi ndio Commissioner yule amekuja washughulikia leo. Asante.

Francis Wachira: Ndiye ametumwa na Professor Yash Pal Ghai ndio mmoja wa wale ishirini na tisa, wale mawakili walikuwa wanazunguka na amekuja hapa kwa sababu wakati tulikuwa hapa, Commission ilisema ile maoni tutapatiana na iko hapa kwa hiki kitabu. “Dr. Mugo can I have this?” Mambo yote ile watu wa Laikipia West walisema iko kwa hii document, ile tulisema Rimuruti, tukasema Nyahururu hapa, tukasema kinamba imerudi kwenu na Commissioner will go through the draft with you ili muone kwamba it a true proceeding of what we told them. So sasa nafikiri kazi yetu itakuwa rahisi kwa sababu tutamsikiza na ningetaka Chairman wa Laikipia West aongee kidogo halafu amwalike Commissioner atusomeshe siku ya leo.

Peter Waweru: Chairman Laikipia West: Asante sana bwana coordinator wa Laikipia District Constitution Review Commission. Ningependa kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wakazi Laikipia Magharibi i.e Laikipia West kumkaribisha Bwana Lenaola ambaye ni mmoja wa wale ma-Commissioner ishirini na saba. Ametoka Nairobi, alifika hapa kabla ya wengi wetu kwa hivyo mnaona kujitolea kwake.

Pia ningependa kumkaribisha bwana Gitonga na bibi Emmah pia kwa sababu ya kuchukua wakati wao ili kufika hapa, nawashukuru nyote hapa, kwa sababu ya kuja ili muweze kuangalia kama kweli yale mambo mliopatia hawa yalitiliwa mkazo ili kutoa draft ya Katiba ambayo wengni wenu mnao.

Mimi kwa niaba ya committee, ningesema nina shukrani sana kwa nyinyi yenu yote kwa sababu tulipoanza ilionekana kama itakuwa ni kazi ngumu lakini nafikiri wamefanya kazi kubwa kuweza kutupatia draft kama hii. Mnajua pia kwamba draft hii ni wengi sana ambao hawako opposed with, wengi ambao wanaingilia, hawapendi kuisikia lakini kwa sababu maoni ambayo yako katika draft hii ni maoni ambayo yalitolewa na nyinyi na sisi wote katika taifa la Kenya. Ni muhimu sana tuweze kuangalia, tujue kweli mambo ambayo yako hapa ni yale tulijadilia.

Nafikiri mkutano wa leo, utakuwa ni wa dissemination, in other words bwana Lenaola hapa atatupeleka through document hii ile atuambia mambo yaliyo hapa na akisha maliza itakuwa ni jukumu letu kuuliza maswali kama kuna mambo ambayo mungependa yawe utapewa nafasi ile. Kwa hivyo, nakumbuka, Commissioner alituambia wakichukua maoni yetu wote mwishowe watakwenda katika kila sehemu ya Bunge ili kuweza kuuliza wananchi ama kutoa. Mnajua, wale mnaofanya mikutano, nao mkisha kutana au mnapokutana tena, mnasoma minutes na kuuliza whether is it a true record of what you transpired, I think that is what you are suppose to do this morning, so that we shall be in a position to ask the Commissioner whether all the things we told him are here and then be in a position to look at this document and ask questions.

So Laikipia West, today we ask the Laikipia East and other Commissioners are missing people in various constituencies so it's a very very important day for all of us. Therefore I welcome all of you to this session and I hope by the end of the day we shall have had a very beautiful discussion. Thank you very much.

Again let take this opportunity to welcome Commissioner Lenaola to tell us or to go through the document so that tuweze kujua kweli mambo tuliongea, bwana Commissioner.

Com. Isaac Lenaola: Asante sana bwana chairman. Jambo la kwanza ningependa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Tume na kwa niaba yaTume yenyewe, tuwashukuru sana watu wa Laikipia West, kwa maana maoni yenu interms of number, one quality the highest in the country. Mjipigie makofi.

Com. Isaac Lenaola: Infact in the country, Laikipia West is only second interms of the number of memorandum which the Commission received. You are only beaten by Nyando constituency, kwa hivyo kazi yenu ilikuwa nzuri sana, kama tungekuwa na medal mungepewa ile inaitwa(?) medal kwa sababu kazi yenu ilikuwa nzuri sana.

Jambo la pili ningependa kushukuru kamati, kushukuru coordinator na mdogo wake, maana kazi ya constituency ya Laikipia

ilikuwa nzuri sana sana, kwa hivyo again kwa niaba ya tume, ningependa kuwashukuru sana.

Jambo la tatu, nilipokuwa Laikipia Rumuruti na nilikuja hapa lakini mkutano haukuendelea. Tuliwaambia kwamba, baada ya kuchukua maoni yenu hatuketi Nairobi ama Mombasa kuandika constitution na kuweka Nairobi, tutarudi hapa hapa kwenu Laikipia ili mtuambie kwamba hii draft ni sawa kwa maoni yenu. Maanake, sheria inasema kwamba the Commission must write a draft constitution which(?) truly reflect the wishes of the people of Kenya. Hii ripoti ya Laikipia West must be equal na hii draft constitution. Maanake hii Katiba ni ya tume, President, parliament na wananchi ya Kenya. So nimetimiza ahadi yangu kwamba, tutarudi hapa hapa kwenu na kudiscuss hii draft pamoja na nyinyi.

Jambo la nne, hii ni draft, there is final proposal, hii ni draft pekee yake, kwa hivyo si kama Biblia wala Quoran haijakuwa(?) stone na pengine kuna makosa, pengine kuna mambo mazuri leo, mtaniambia kwamba kuna makosa mahali fulani ama kuna jambo mahali fulani tutachange. Na watu kama Pascalina, wakija kwa National Conference kazi yao pia ni kuchukua hayo maoni yenu na kupeleka katika National Conference kwa hivyo, msione kama hii ni mwisho wa dunia, hapana. Mtakuwa na nafasi baada ya kuzungumzi kuniuliza maswali ya kufafanu ama kujibu maswali ambayo hayako clear. Mtaniruhusu nizingumze kwa Kiswahili na Kiingereza nafikiri ni sawa pia. Maanake Kikuyu yangu ni ile ya kuomba maji si nzuri sana.

Hii ripoti ya Laikipia West itakuwa kwa ofisi ya province na pia council ya Nanyuki mtasoma muone vile mlisema. Kazi yangu ya leo ni kusema hii, mlisema nini Laikipia na je hayo mambo yako kwa hii draft ama hayako? Kama hayako ni kwa sababu gani. Kwa hivyo, wale ambao tuko na draft, tutachukua. It is a very big document with 299 article and almost a hundred pages. Kwa hivyo siwezi kwenda article by article. Nitachukua mambo ambayo ni muhimu kwenu halafu tutazungumzia hayo.

Jambo la kwanza, mlisema kwamba mungependa hii Katiba iseme kwamba watu wa Kenya ndio msingi wa taifa, supremacy and sovereignty of the people of Kenya.

Kwa hivyo at stage number four of that document, chapter one article one page four inasema. All sovereign authorities belongs to the people of Kenya. Nguvu zote za nchi zitakuwa katika watu wa Kenya, ziko rights, parliament, ziko kiti lakini sovereignty belongs to the people of Kenya. Kwa hivyo mlisema hivyo na kisha mlisema kwamba in the memorandum was that the preamble should provide for sovereignty expressing, sovereignty of the people.

Halafu the people of Kenya must be sovereign. We have captured that in article one in the same language that you said it.

Jambo la pili, mlisema kwamba, ijapokuwa watu wa Kenya watukuwa ndio wenye nguvu zaidi kusema. Kila mkenya, kutoka mkubwa mpaka mdogo awe chini ya Katiba. Zamani ni kama wanakenya wako chini ya Katiba Rais yuko juu ya Katiba. Mkatuambia kuwa mkenya kutoka President mpaka chokora awe chini ya Katiba na Kenya iwe nchi ya kuongozwa na Katiba.

Article two page four, the constitution is the supreme law and bind all the authority and persons throughout the republic. Katiba iwe juu ya kila mtu Kenya, na msiwe na mtu ambaye ako juu ya sheria wala juu ya Katiba. Kusema ukweli hivi sasa wakenya wangependa kwamba hii Katiba ipitishwe na wananchi waende kwa election chini ya hii Katiba. Lakini out of 30 milion Kenyans, one person can afford to say that is all nonsense. Maanake sheria sasa vile iko, sheria ya Rais ina nguvu nyingi sana kariba hata kupita Katiba yenyewe, kwa hivyo tumesema kwamba kwa hii draft, Katiba ndio sheria kubwa zaidi katika nchi ya Kenya.

Jambo la tatu Laikipia mlisema kwamba pale Kinamba, nilikuwa Kinamba mnakumbuka Pastor(?) nilikuwa Kinamba na Professor Okoth Ogendo na mwenzetu Alice Yano. Na jambo kubwa katika Kinamba na Rimuruti ilikuwa security, what is it they are saying about the security? Let us turn to article 41 page 7, third column it says everyone has a right to freedom and security of the person. Haki ya ulinzi ya kibinafsi, i.e. right of the security of the person.

Article 43 page seven column number four days, every person has the right to privacy which is the right not to have their persons or home searched, their property searched, their possession(?). Haki ya kutoingiliwa, haki wa kutodhulumiwa, haki ya mali yako na ya nyumba yako kutoingiliwa bila mtu kuwa na.....(?).

Hivi sasa mnajua polisi akija kwangu ama kwako, anabisha, kama hufungui anaingia na mlango. Hakuambii kwamba niko na idhini fulani ya kuingia kwako, anaingia na nguvu na mlango ama kwa dirisha. Tunasema kwamba mtu awe ni polisi or mtu mwingine akitaka kufanya search kwako lazima kishiria awe na wewe.

Haya article 54 page number 8, last column says 54, every person has a right to acquire and own property either individually or in situation of others. Haki ya kuwa na mali yako kivyako, iwe ni wewe binafsi ama mkiwa wawili. Na mlisema kwamba Laikipia mngenda mkenya awe na haki ya kuwa na mali mahali popote nchini Kenya. Manake ukiwa mkenya hujaambiwa uwe mkenya wa Laikipia peke yake, ama Mkenya wa Kiambu uwe peke yako. Umekuwa mkenya katika nchi nzima ya Kenya na lazima mali yako pia iwe imekuwa protected na hii sheria.

Haya article 264, page number 32, mlituambia hivi, kwamba mngenda polisi specifically waambiwe kwamba kazi yao katika nchi ni usalama kwa watu. In article 264 sub article 1C, the primary object of the Kenya police service is to work with and for the people to ensure the security of the people. Kikatiba kazi ya polisi ni kuona kwamba kuna usalama wa watu wa Kenya. Kwa hivyo kwa hii draft, tumewawekea mambo ya security vile mlisema.

Jambo la nne, Laikipia mlikuwa na maoni tele kuhusu vyama vya kisiasa, political parties, mkituambia mngenda kuwa vyama visiwe vingi Kenya. Na funding itoke kwa serikali. Mkasema kwamba hizo fedha za party zitumiwe kikamilifu.

Mambo matatu makubwa, tukashughulika kama kundi tukaona kwamba if we limit the number of parties then we are limiting a principle called right and freedom of association, tukasema hivi article 87 page number 12, last column. In accordance with article 50 any person may form a political party, huwe na haki na uhuru wa kuwa na chama chako cha kisiasa. Lakini katika hiyo article, tumesema kuna masharti fulani mambo ya chama lazima iambatane nayo. Kwa hivyo at page number 13 article 90, tumesema kwamba masharti A, B, C, D ni lazima chama ishikilie na iweke manani, kwa mfano article 90 sub article 2, the Commission shall not register a political party if that party is found purely on the religious, linguistic, racial, ethnic, sex, cooperative or regional business. Kwa mfano, kwa nini tuwe ambacho kinaitwa chama cha akina mama wa Kenya, hiyo ni chama cha kisiasa? Ama chama cha Wasamburu pekee yao, ama chama cha Kinamba peke yenu, haitakuwa chama ambacho kiko na national outlook.

Tusema mimi ni Mwangilikani, tuseme the Anglican party of Kenya, itakuwa kanisa ama chama, ama the Catholic Party of the kinamba Parish Party, haitakuwa chama tena, haitakuwa kanisa tena. Tukasema vyama viwe na kiwango fulani na kiwango ni kwamba they must have a national outlook.

Na je ni kwa nini tunaweka vyama katika Katiba? Kwa sababu hivi leo mambo yanayofanyika Nairobi, je ni ya demokrasia kweli? ni democracy? Manake tunawacha vyama viwe na internal management ya mambo yao, na wakifanya hayo wanafanya.....(Inaudible) haifuati sheria tukasema they must manage party within the frame work of the law. Lazima vyama viwe chini ya sheria pia. Maanake, kila mkenya ako kama (sawa na) kwa hivyo chama iwe chini ya sheria.

Na je kama vyama vitapewa pesa kutoka kwa serikali watazitemia namna gani? Article number, 95 page number 13, money allocated to a party from the political parties fund shall be used only to cover:-

- a) Election expenses of the party i.e., zitumiwe kwa minajili ya elections ya chama.
- b) For the organization of the party of civic education in democracy and the electoral process, you will agree with me kwamba civic education kwa hii Katiba ya Kenya iliwafungua wakenya macho, imewafungua wakenya vichwa wameona kwamba haki zao ni zao. Na tunasema vyama vya kisiasa, somebody's vehicle for civic education. We shall fund them to do civic education. You have got the chance, mlituambia Laikipia kwamba mngenda serikali ya karibu, hamkupenda nyinyi watu wa Laikipia West kwamba Serikali iwe serikali wa mbali. Infact, you said in Laikipia that you would like the provincial administration to destract and two you would like the Government to be brought to local levels.

Artilce 213 page number 26, second paragraph, chapter ten talks of devolution of power, nguvu za uongozi wa inchi uje chini karibu na wananchi. Article 216 last column, powers are devolved to the following levels:-

- a) The village.

- b) The location.
- c) The district.
- d) The province.

But what is the centre of power, the centre of power is this constitution in the district, not the province, the central government but the district i.e. Wilaya.

Article 218 talks of the district government, serikali ya wilaya. Mkatuambia hivi, hamngependa kuwa na DC ambaye hamjui ndugu zake wametoka wapi. Mlisema mngependa mtu wa district awe mtu wa kuchunguliwa na wananchi wenyewe, maanake sasa nimesikia kwamba leo DC anakuja after two weeks yuko transfer.

Audience: Ndio.

Com. Isaac Lenaola: Hata bila kukutana na watu. Mwingine anakuja every Wednesday kwao ni Migori, Wednesday Migori, Monday Nyahururu. Hamuoni for four weeks maanake he is not available to you.(?) not come from you it comes from somebody else. Ama ni rafiki wa PC na(?) kwamba amefanya PC kila wiki anataka mbuzi. Kwa hivyo kama ni Msamburu kila wiki yuko barabara ni akitafuta mbuzi ya PC Samburu, hafanyi kazi wananchi mahali ametumwa.

Tukasema hivi article 218, 4 the district administrator is elected directly by the voters of the district. Mkubwa wa Wilaya apigiwe kura moja kwa moja kila miaka minne na wenye kura katika hiyo district. Tusikuwe na mtu ambaye hatujui mahali ametoka, hamjui kama yeye ni mkora kwao, ama aliiba mbao district fulani, ama alikuwa ni mtu ambaye mambo yake ni kombokombo district fulani, mnaangushiwa tu pa! anakuwa Distric Commissioner, tungenda kwa hii Katiba kwamba awe(Inaudible).

Na je hivi sasa PC akiwa kombokombo wewe unaweza kumchukua wewe?

Audience:(Inaudible).

Com. Isaac Lenaola: Hata kama akija kuwatusi kwa mkutano, kuna jambo utafanya?

Audience:(Inaudible).

Com. Isaac Lenaola: Tukasema hivi, article 218 sub article 6, the district administrator can be dismissed by the vote of an absolute majority of members of the district council, that he is supported by the memorandum by a majority of both bodies in the referendum. Akiwa mkora, akiwa mlaghai district council yaweza kupiga kura kumtoa huyu district administrator. Lakini kwa vile si wao wamempigia kura pia hiyo vote yao ije kwetu kwa wananchi. Tusema kwamba we shall

be.....(Inaudible) or not we shall not be.....(?). Kwa hivyo sasa huyu district administrator atakuwa chini ya amri ya wananchi wa hiyo district. Si amri ya PC, amri ya PS internal security, ama amri ya the ministry of Internal security ama amri ya President bali atakuwa chini ya amri ya wananchi wa sehemu ile ya wilaya amechaguliwa ndani, si hiyo ni safi?

Audience: Hiyo ni safi.

Com. Isaac Lenaola: Jambo lingine ambalo ni muhimu katika mambo ya kiongozi wa Serikali, article 226 page number 27. Inasema hivi district shall be entitled to a substantial share, of natural resources from local revenue and for the location of a 50% to the communities in whose areas the resources are generated. Ndani ya wilaya, usiende Nairobi upigiwe na wale wakora wa Nairobi, ndani ya wilaya ibaki kwa wilaya kiwango, lakini kidogo iende kwa national coffers kusaidia mambo ya nchi, lakini percentage kubwa ibaki hapa.

Na pia katika wilaya some percentage iende mahali hiyo resource imetoka, hakuja haja for example kuwa na forest kama hii ya Nyahururu halafu hii forest wakitaka hiyo miti kuuza hiyo revenue inapelekwa ministry of natural resources Nairobi. Na watu wa Maina why conserve the forest everyday don't get a single shilling from the forest.

So tunasema kwamba a portion must also remain kwa wale wenye kuchunga, ama wanyama wa pori. Tourisms, they say is the highest earner of the foreign exchange in this country. Na kuna watu wanaishi na hao wanyama daily. Kama ulikuwa unanua hiyo nyama na kukula kila siku what(Inaudible)? So we are saying let those who conserve the resource also benefit from that. Lakini kuja kuwa Laikipia for example pesa za wanyama watu wa Laikipia hawakuli ndovu, hawakuli punda milia na Wazungu wakitoka ng'ambo na ndege kuja kuona punda milia Laikipia na hizo pesa hupita Nyahururu, zinapita Naivasha pia to Nairobi.(Inaudible) na mwenye kuchunga hapati ndururu. So we saying let us share remain where the resource is.

Haya, jambo lingine Laikipia mlisema hivi, mambo ya Bunge and I am just going through juu juu siendi ndani ndani maanake you will read the document. Nilisema kama kuna any question I can answer later, but I am saying let me just speak on the important point then have time for debate.

Mambo ya bunge, Laikipia West you had a lot of views on parliament, parliamentarian, what to do with an MP, mishahara ya MPs. Tunasema nini katika hii document, article 101 page number page number 14. Laikipia West you were such(Inaudible), that you don't want the President to be the sole appointee of high Government offices; you were very keen on that, mlisema?

Audience: Yes.

Com. Isaac Lenaola: Any appointment must be vetted by parliament so that one person cannot appoint at 1.00 o'clock and suck the next day at 1.00 o'clock. Maanake sisi tunasikia hao wakubwa wakitembea wakienda na kale ka radia kadogo ile small radio ile inatwa Philips kale kadogo, na ikifika five minutes to one wanafungua kwa sababu you don't know whether you are going to be in the office or not.

Pili am told now ministers kwa ofisi yao all the personal cheques are not from a drawer or from a shelf iko kwa box ndio ukiambiwa hora unahora.....(Inaudible) (*Laughter from the audience*).

So we are saying this let parliament approve all senior appointment.

Article 103, we are saying, second paragraph the national council must approve appointment of all the Commissions, be it(Inaudible) ethics Commission, land Commission environment Commission, teachers service Commission, salary Commission, Attorney General, Judges and Kadhis.

Second line, national assembly will have to approve Prime Minister, deputy minister, ambassador, Commission, controller general and governors of central bank. We are now saying all offices which are constitutional must be approved by the national assembly or the national council, so that one man cannot have the power to hire and to fire.

Two, in Laikipia, you told us you would like two houses in the Parliament, a lower house and upper house. Article 105 paragraphs 3 page 14. There shall be two houses of parliament an upper house called the National Council and a lower house called National Assembly. The reason for this is that mumeona kwamba kuwa na nyumba moja bunge, you also become law unto themselves, they can pass law if they want or reduce that law if they don't want.

So we are putting a house to check the lower house and upper house kuchunga hii lower house na upper house nyumba ya wazee. "I am just going to be 35 years in December and I don't qualify now to be in the upper house." Because sijakoma miaka ya kuingia upper house, sijakuwa Mzee," nikasema kwamba upper house let the members be 35 years and above. The lower house let the members be 21 years and above, so that wazee wachunge vijana kwa lower house maanake tunaweheshimu wazee. Kwa hivyo mlisema hayo na tumeandika.

Na je kuna mambo mingi juu ya election ya Member of Parliament and so on, but let me just pick one point which you raised in Laikipia. Article 111 page number 16, mlisema hampendi mbunge ambaye mnamchague kwa tikiti ya DP akifika bunge anapewa million ngapi, anaambiwa wewe si mtu wa DP tena wewe ni mtu wa KANU, lakini tikiti yako ni ya DP. Niwape mfano mmoja, kuna Mbunge wa Likoni constituency anaitwa Mheshimiwa Suleiman Shakombo. Mheshimiwa Shakombo alichaguliwa na tikiti ya Shirikisho akaingia Bunge na tikiti ya Shirikisho kabla ya miaka mitano, akaenda kwa chama cha KANU akapewa life Membership certificate ya KANU na mjue kwamba contract yake na watu wa Likoni go thee to

Parliament and represent us on the Shirikisho ticket, so mguu moja uko kwa Shirikisho mwingine uko wapi? KANU, tukasema nini article 111 is(Inaudible). If the member leaves the political party for which the member stood as a candidate for election to parliament, he joins another party or to remain in parliament as a member that office shall become vacant. What are you trying to suggest? We are saying there shall be no unclear defection, ukidefect(Inaudible). Go back to article seven, nyinyi mlinichagua kwa Shirikisho lakini mimi Shirikisho mambo yake mimi sioni mimi napenda KANU damu nichagueni kwa tikiti ya KANU, come back here we vote for you again, but don't stay in parliament for five years against our will in the wrong political party.

You are still in the last one year you are not very sure now how many members each party has in Parliament because there prone defections. My friend Shem Ochuodho MP for Rangwe, NDP was killed hakuvingia KANU akaingia SDP hakufurahi huko, akanunua(Inaudible).....(Inaudible). So in six months you transient four or five parties and yet we told you, go(?) to parliament and represent us on this ticket. So we are saying huo mchezo wa kuhamahama ukwame maanake hii draft imekataa.....(Inaudible) ni kama prostitute unajua mimi ni mtu wa heshima na akina mama wako mambo kwa hayo mimi sisemi.

Article 14 page number 16 subject to this article, the electorate of any constituency has the right to be recall their member of parliament before they expiry.....(Inaudible) of the term of parliament, mlituambia hivyo. Hampendi kwamba mbunge akichaguliwa bas! miaka mingapi?

Audience: Mitano.

Com. Isaac Lenaola: Whether he(Inaudible), whether he is sleeping, whether he doesn't sleep miaka mingapi?

Audience: Mitano.

Com. Isaac Lenaola: Let me give you an example, a few years back in Moyale constituency in Marsabit district, mjumbe mmoja alipiga campaign something moja kali, I will bring you schools, sijui barabara amesema ni mbaya nitawatengenezea,(Inaudible) mambo ya cattle rustling itaisha. Watu wakampigia kura(Inaudible) constituency, the day he got elected akawaambia bye bye sitawaona tena, the man never went to the constituency till five years, akahamisha familia yake from Marsabit akawapeleka Mombasa, akafungua clearing and forwarding firm in Mombasa, kazi yake ni Nairobi, Mombasa, na Moyale iko Mombasa kweli? Moyale iko Nairobi? And for five years they never saw him and the man has not gone back to Moyale in the last fifteen years.

Now,(Inaudible) in those five years si at least they would have recalled him?

Audience: Yah.

Com. Isaac Lenaola: But there is no law so we are saying here in article 216 a member can be recalled on any of following ground: -

- a) Physical and mental in the party.
- b) Misconduct.
- c) Persistence desertion of the electorate, siukihama watu wako, si basi uhame kabisa ujitolee. Hauna sababu ya kuchaguliwa na haufiki constituency so you note the issue of recall a member or parliament.

And the reasons for this it that MPs must become responsible to those who elected them.

Pili, if a man is so sick that he cannot perform the duties of an MP why should he stay there for five years. Unakosaje kuwa mgonjwa kweli, lakini kama wafanyikazi maanake ni mgonjwa basi we shall take your post. There are two MPs now in this KANU parliament who have not left their houses or hospitals for two years, they don't go to parliament, they don't go for meetings because they are sick. If you become sick for Gods sake supervise but you must come back personally and work for the people. Haya, mlituambia hivi hampendi Wajumbe wajiwekee mishahara yao because the principle of employee means that if you are an employee you don't check your own salary. Wewe ukiwa mfanyikazi mahali uko sasa huwezi kaa chini ukaambiwa leo kazi ilikuwa mingi bwana nitajiongezea 200%, without consulting anybody. In the last two years the current parliament has given themselves three mishahara rings. Ya kwanza ilikuwa ile cash, right now a minister earns close to a million shillings per month. *(End of tape I Part A.)*

Speaker:(Inaudible).

Com. Isaac Lenaola:(Inaudible). From that day there is no different between opposition and KANU, NDP, KANU, DP, SDP they had for the first time a clear understanding issue. They agreed mishahara ipande na ikapanda, ile mambo ya party differences sijui Rainbow, sijui Project ilikwisha siku hiyo, mishahara ipande 200% ikapanda. The second time, they gave themselves insurance policy each of them insurance of 10 million shillings, they never asked anybody na pia hakuna mambo ya hati wewe wewe ni mtu wa Kibaki, wewe ni mtu wa Moi hapana, mishahara ikifika ifike.

The third one they gave themselves mortgage facilities 10 million kila mmoja, they never asked anybody, so we are saying article 151 a Member of parliament shall be paid(Inaudible) salary allowance and benefits and will be determined by salary and remuneration Commission,(Inaudible) inje ya bunge kupanga mishahara allowances na benefits za wajumbe. Hiyo ni safi?

Audience: Ndio.

Com. Isaac Lenaola: Maanake(Inaudible) other Commissioners decide because I have got gray since I got to the Commission, I must pay myself a 100% rates, that not myself. Kwa hivyo mlisema hivyo na tushaweka.

Haya mambo ya Rais wa nchi: article 156 page 20, second column, one thing Kenyans were very clear about is that the Presidency is too powerful, the sitting President infact in 1999 said in public, my office is too powerful sometimes I say I have too much power, but it is true. Mwenye kiti mwenyewe amekubali kwamba mumenipa nguvu nyingi sana, mkatuambia hivyo.

Next the powers of the President(Inaudible) let those powers be discussed; right now we are teaching what referred called a constitutional dictatorship. We have given one office, Constitutional Dictatorial. Why do you have a Katiba, which says the President may dissolve parliament at anytime.

You are giving one person more powers over elected leaders of the ministry. Parliament is an elected by Parliament but one person has the power to tell those leaders go without consultation. Then you told us rights in the constitution, that the powers of the President must be reduced.

Article 156, we have given to that article all the qualifications for the President, article 151 second column, states functions of the President and article 152 legislative functions of the President, let explain in it in brief. What we have done in this chapter we have made the President less powerful in the following manner, when Presidents appoint somebody parliament must vet.

Two, we are saying let the President be the head of state i.e., Mkuu wa nchi but not the head of parliament, si mkuu wa serikali. The republic iwe na mkubwa wake lakini serikali iwe na President Tumegawa nguvu because right now we have a President who is the chairman of the party, he is the head of state, he is the head of Government, Commander in chief .

Speaker: Councilor.

Com. Isaac Lenaola: Hata hiyo ni yake.

Speaker:(Inaudible).

Com. Isaac Lenaola: Farmer number one, fisher number one, so in one person we have literally the entire country and bought.....(Inaudible). We are saying those powers must be cut, so that each power can take the other. So that mambo ya kuwatch news iishe, na radios ikose market maanake mambo ya kununu radio kilasiku

kungoja news sio yako, we buy other things not just radios.

Precisely we are saying let us have this scattered. Article 150(?) the President shall not hold any other public, including any elected or appointed office within a political party. Let the President be the symbol of the nation, asiingie mambo ya vyama, asiingie mambo ya Agricultural society of Kenya. There is a minister for agriculture afanye mambo ya agriculture. President afanye kazi ya nchi hapana kufungua show. So we are saying let there be clear separation of power.

Haya jambo lingine mlisema kwamba, hamngependa President ambaye(Inaudible) kura zake zihesabu ni 20% ya national votes, let the President be popularly elected.

Article number 157 sub article four paragraph three explains this. Candidate for President who receive more than 50% of all the voters cast in the election and in addition he receives a minimum of 20% of the votes cast in more than half of the provinces shall be elected the President. What are we saying? We are saying let the right President awe popularly elected across the nation, you are telling us let them be elected at 50% of the votes and 20% in five provinces, we amended your proposal to make it more realistic and we are saying 20% to how many provinces?

Audience:

Com. Isaac Lenaola: So yenu ilikuwa 50% and 15% in five provinces, we slightly amended it but basically your proposals imeingia.

Haya Makamu wa Rais: As we speak now, we have no Vice President and yet our present Katiba says there shall be a Vice President of the republic of Kenya. When we say shall, it means what?

Audience: Lazima.

Com. Isaac Lenaola: Lazima kweko, so kama hamna Vice President mumevunja Katiba ya sasa and the person who also appoint the Vice President is therefore frauding the constitution, because it says there shall be, lazima kuweco Makamu wa Rais kwa nchi. And why we are not able push it is because a gain it is the right and role of one person to appoint the vice President, what have we done there? We have said in article 165.

Page 21 paragraph two, each candidate in a provincial election shall nominate a person duly qualified for election as the President and a candidate for a vice President. When you say, "I want to be President" you must nominate somebody else who has the same qualifications as yourself to becomes vice President as your running mate. We vote for the President and the VP together. Let me give you a small example why this is important view and why the Vice President must be qualified as

President. Because if God forbid the President collapses today, who shall become President?

Speaker: The Prime Minister.

Com. Isaac Lenaola: You will have serious crisis of the constitution so we are saying, because we are thinking a head not thinking mahali ya kula peke yake, we must have a vice President who is as qualified as the President. So that if anything to this one, we have a qualified person to hold the government until new election is held. Hiyo ni correct procedures?

Audience: Yes.

Com. Isaac Lenaola: So we are saying the Vice President must not just be an office where you put your friends unawaambia kwamba you are my friend for 13 years so I may give you so I may be your Vice President, so now I am not your friend anymore you cannot become Vice President. This is serious thing, not about friendship. This is a serious constitutional issue.

Haya haki za kibinadamu, article number 29 page 6, mlituambia hivi, kuna haki ambazo mtu ako haki za kibinadamu, hazipewi na mtu Fulani, hupewa na Mungu. Article 29 sub article 15, the right and freedom set out in individual rights belong to each individual and are not granted by mistake. Hatupewi hizi haki na ni nchi za serikali tunapewa na Mungu, manake mimi ni binadamu. Mlisema pia kwamba the state area not going to take away our rights. Serikali, haiwezi kuchukua hizo haki kutoka kwa Mkenya maanake iko katika damu, ni za utu, kama damu.

Article number 32 paragraph three, the same page, everyone has the right to life, haki ya kuishi sasa hiyo utapewa na serikali ama na MP, ama na PC.

Speaker: Hakuna.

Com. Isaac Lenaola: Maisha ni upewa na Mungu.

Speaker:(Inaudible).

Com. Isaac Lenaola: Kwa hivyo serikali haitupatia sasa wewe ishi leo kesho ukufe, ni kama huna.....(Inaudible), kama nakuandika leo nikufute kesho, hapana, serikali haina haki kwa maisha ya mtu. Tumesema article sub(Inaudible) the death penalty is abolished, why are we saying that, because even if umefanya makosa kubwa ama jambo haki ya maisha si haki ya serikali wala mtu mwingine.

Haya article number 35, akina mama furahini tumewakumbuka kwamba akina mama pia wakae na haki zao. Article number

36, wazee mfuarahi tumesema kwamba all the members of the society shall enjoy the right and trying to make constitution. Ni nzuri right to pension and a fair pension. Ni aibu if you work for a government 30 years, when you retire they tell you your pension is 340 shilings and for the next 40 years anakula 340 shillings, pension.....(Inaudible). So we are saying let the wazee have pension which is equitable to somebody living vile maisha inaendelea, wawe na haki yao ata moja.

Article 37 next page, haki za watoto, mumetuambia hampendi chokora, hampendi watoto ambao wanaumia umia, wapewe haki zao. Sub article two na hii ni ya wazee na vijana, mara nyingi mnamangamanga, mnaza halafu mnaambia mama mtoto ni wako, hakuna mtoto wa mama peke yake, sub article two, all children whether born within or outside wedlock are equal before the Lord. Watoto ambao wamezaliwa inje ya ndoa ama ndani ya ndoa wawe na hiki zao.

Sub article four na wazee hampendi hii sana lakini tumeandika katika Katiba yetu, a child mother or father whether married to each other or not, has an equal duty to protect and provide for the child. Kwa hivyo msifikiri kwamba mtazalia Njeri Kiramba, mtazalia Wanjuku Rumuruti, mnazalia Nyambura Nyahururu mtoto si wako ukimuo Njeri ama Wanjiku, ama Nyambura mtoto ni wako(Inaudible) na uko na duty kisheria kumtunza huyo mtoto, mnaelewa kwa hiyo, kama hampendi ni Katiba. *(Laughter from the audience).*

Haya article 38 haki ya jamii, tuwe na haki ya jamii. Article 39 haki za watu walemavu, maranyingu tumewaka hao nyuma tukasema kwamba katika hii Katiba wapewe haki zao.

Article 55 page 9, na kama kuna walimu mtafurahi kusikia hii kwamba sub article two every worker has the right to a fair remuneration, haki ya kuwa mshahara mzuri, sub article two, the right to reasonable working condition, sub article three, to join trade union, halafu walimu watafurahi the right to strike, kwa hivyo kama hii Katiba ingekuwa saa hizi inatumika walimu mngekuwa within the law when you go on strike, because the law says the right to strike is a fundamental human right, because you only way you can tell your employer unless you negotiate with me I will not perform my work well. It is interesting here, how can any person, any employer enter into an agreement with an employee and then without consulting the employee, throws the argument through the window? It is immoral unjustified and illegal(Inaudible).

Haya article number 57 the right to health, haki ya kuwa na Afya njema, article 58 the right to education, haki ya elimu, 59 haki ya kuwa na nyumba, 60 haki ya chakula, 61 haki ya maji.

Article 3A language and culture, haki ya kuwa na lugha yako na mila yako. Article number 68 section page 9, the right of arrested person. Tunasema hivi, mara nyingi watu hushikwa unatupwa ndini hupelekwi kortini, hufunguliwi unakaa ukila tu unga na maharagwe. Tunasema hivi, every arrested person sharti aachiliwe within 48 hours ama apelekwa kortini. Na hizo Article zote huzungumzia mambo kama hayo.

Katiba ya sasa chapter five, iko na haki nyingi, lakini hakuna njia ya ku enforce hizi rights, but there is no mechanism for enforcement of your right, in the present constitution. What are we saying here, article 23 page 11, a person listed in this article has the right to complain to the Commission on human rights or approach a code of persons decision alleging that a right has been denied, violated, impeached, oppressed. There is no Commission that iko katika hii Katiba i.e. the Commission of human right. Page 35 column two article 288, there shall be a Commission on human right we shall a Commissioner on human right and the people protector na huyu ataitwa ombudsman, mlituambia tuwe na ofisi ya kupeleka malalamishi yenu. Manake sasa polisi akikunyanya hati kwa DCS na OCS na pia ni polisi ama OCS akikataa uende kwa OCPD ni polisi.

Audience: Ni polisi.

Com. Isaac Lenaola: So we are saying let pass an independent office in every district ambayo malalamishi yako. Jambo la pili, nimesema kwamba kuwe na korti ya kupeleka malalamishi juu ya thulma, kuhusu haki za kibinadamu. Lakini sasa hayo tumesema. Mimi ni Wakili na mnasemanga hapa Nyahururu mna mahali pengine oh mawakili ni mkora, oh wanakula pesa ya watu wao hawaendi kortini na anakula pesa, tungependa kuwe na Wakili, ambaye hatulipi kwa kupeleka mambo yetu kortini. Article 210 page 26, there will be the office of the public defender, mtetezi wa watu, sub article four, the defender shall provide legal advice and representation to person when unable to afford legal services. Kwa hivyo tulisema kwamba watu kama mimi biashara, hakuna kwa sababu sasa kuna Wakili wa Serikali Wakili wa wananchi.

They cannot say. "I cannot go to court because I have no money" there is someone to take you to court and advice you for free kama haki zako zimefinywa kwa njia fulani, hiyo ni tamu sama?

Audience: Ndio.

Com. Isaac Lenaola: Kwa hivyo Mawakili sasa tuwache ukora, kwa maana kuna competition kwa kazi, eh.

Audience: Mumekula sana.

Com. Isaac Lenaola: Tumekula zaidi, haya. Hii Katiba iko na mambo mengi let me just pick on one point which you raised in Laikipia a list that came out from Rimuruti and Kinamba. Page 28, article 235 the last column, we are saying this, mambo ya ardhi, kuna watu amboa walikuwa sasa na clashes Molo, clashes Njoro, clashes(Inaudible) clashes mahali pengine.

Kuna pia claim kwamba mashamba ziko na tenants katika Laikipia, tumesema hivi, within two years parliament shall enact law and article sub E2 to provide for the review and assessment of all claims transact, extra creation in the Coast, North Eastern and Rift Valley provinces or elsewhere whether arranging from Eastern province or other provinces in order to establish the

validity and how fresh they can be justly, peacefully and equitably resolved. Mambo ya mashamba iwe juu ya clashes, hata Wazungu wamesema kwamba tuwe na mechanism ya kuresolve hizo matters peacefully and physically ndio kila mtu awe na haki kwa ardhi yake.

Kuna mashamba yalichuliwa, maploti zimechukuliwa na land grabbing, what are we saying here above that article the review of all land or dissolution of government and other public land to establish a society and legalism and to establish whether or not such land should be resolved. If somebody has grabbed land there is no sheria tumesema kwamba, you must investigate and see kama itakuwa revoked ama(?). We have addressed those concerned in this draft constitution.

Nikiendelea kumalizia je and I have just told you that hii draft iko na article 299 I have just picked out some that I think are very important kwenu watu wa Laikipia na kuna zingine nyingi mtazisoma na mtume maoni. Hii Katiba ni ya nani? Page number two, article inasema hivi, we the people of Kenya, sisi watu wa Kenya, hii Katiba si ya tume ya President, na parliament. Ni ya watu wa Kenya.

Last paragraph we adopt and act and give to ourselves and our future generation this constitution. Tunajipa sisi hii Katiba na vizazi vinavyokuja. Hii Katiba si kura ya 2002, si ya kura 2008, ni Katiba ya miaka na miaka, kwa hivyo sisi wenye tuko hapa tutajiundia hii Katiba na pia tutawaundia wale ambao hawajafika bado.

Na jambo la mwisho God bless Kenyans, Mungu utubariki Kenyans. Kwa hivyo ni Katiba ya sisi tutampatia Mungu pia nafasi na tutawaomba wale wanakuja nafasi kwa hii Katiba. It is a(Inaudible) document; I like calling it an all time document. Ni ya sasa ni ya kesho, ni ya milele.

Nimekumbushwa kama kuna mambo mawili ya kuzungumuzia na ni ya maana. Jambo la kwanza, na hii ni addition sasa nafanya. Article 213 page number 26, let us first go to article 216, Serikali ya village, what is a village in this constitution? Mlituambia hivi hamngenda kuwa na D.O. kwa sababu hamuoni maana ya D.O. mkasema tungenda kuwa na wazee, or you change that the chief should be elected.

Article 216 inasema the village decides whether the council is made up of village elders on election, mkaamua hivyo.....(?) mngependa kuwa na wale Wazee ama mtachagua watu kati council Article 217, location council shall consist of two persons from each village and one of whom shall be a woman.

218, the city council consist of members elected directly by the voters from the district and shall no be more than 30 or less than 20. Serikali ya wilaya is elected directly, the councilors are elected moja kwa moja to the council, mnaelewa hiyo? Moja kwa moja although the district administrator equivalent to the D.C. mnapigia kura na pia councilors, anapigiwa nini?

Audience: Kura.

Com. Isaac Lenaola: For how many years?

Audience: Five.

Com. Isaac Lenaola: And the same principles applies they have the right to be recalled wakimissbehave wana..

Audience:(Inaudible).

Com. Isaac Lenaola: Basi mambo ya wilaya, you told us that Laikipia district is not the same as Kiambu district. Laikipia haina barabara nzuri, Laikipia haina maendeleo mazuri. Je how do you make this district equal to others? Let us start from Article number 213A, the principle and object of devolution has ensured equitable sharing of national and local resources throughout Kenya, we stated provision of marginal areas, we must put funds where there is no development. Hakuna maana kwamba Laikipia haina lami halafu Baringo inaongezewa lami. That every year instead of putting tarmacs in Laikipia you put a new layer in Baring or in Muranga, or in Nyando. We must have equality of development.

In page five sub article 11, the republic shall ensure a fullest participation of women, the disabled and marginal community in the political social and economic life of the country that is very clear.

Article 86 page number 12 is very interesting I like telling you stories because it has a fair view to what Laikipia is now. Tuliambiwa kwamba maeneo kama Laikipia if we were to go by speculation, Laikipia would have one and a half constituencies, now we have two. You told us you want more constituencies in Laikipia, si mlisema hivyo? Kwamba katika West is too big for one member of parliament.

Laikipia East is too large Mheshimiwa Kiangili told us that despite the(Inaudible) cover this constituency kutoka Isiolo mpaka Samburu, from Baringo to Mt. Elgon(?) so we say in this article don't just look at the population kugawa constituency, look at means of communication, geographical features, the communities ambao wako pale and boundary za hapo. So that Laikipia West really should have another constituency.

